**Kazi Muhimu**

***Tokeo Na. 1***

- Kutoa Mafunzo kwa wawezeshaji wa Kata na Kikundi Kazi cha Wilaya kuhusu kujenga uelewa, kuanzisha asasi, upangaji mipango wa jamii, utekelezaji na usimamizi na ufuatiliaji na tathmini.
- Kufanya uchambuzi wa wakufunzi/taasisi za mafunzo ikiwa ni maandalizi ya mafunzo ya uwezeshaji hapo baadaye.
- Kuendesha Mafunzo ya Wakufunzi (TOT) kwa ajili ya Mafunzo ya Wawezeshaji siku za usoni.
- Kubadilishana uzoefu wa kazi kati ya Wawezeshaji wa Kata na wajumbe wa Kikundi Kazi cha Wilaya.
- Kufanya mapitio na kutoa mrejesho kwa ajili ya uboreshwaji wa mfumo wa mafunzo

***Tokeo Na. 2***

- Kuisaidia jamii kusimamia mchakato wa maendeleo yao (kujenga uelewa, kuanzisha asasi, utekelezaji na usimamizi na ufuatiliaji na tathmini).
- Kuifundisha jamii kuhusu mchakato wa maendeleo.
- Kubainisha na kufanya mafunzo ya wawezeshaji wa Jamii watakaotoka miongoni mwa wanajamii wa Vijiji vinavyotekeleza Mradi.
- Kufanya mapitio na kuandaa mkakati wa uenezaji kuhusu usaidizi wa mchakato wa maendeleo katika ngazi ya kijiji.

***Tokeo Na. 3***


- Kuzisaidia Halmashauri lengwa ili kukuza usaidizi wao kwa jamii.
- Kujadiliana na Timu za CMT za Halmashauri lengwa kuhusu mchakato wa maendeleo ya jamii (kujenga uelewa, kuanzisha asasi, utekelezaji na usimamizi, na ufuatiliaji na tathmini).
- Kufanya mapitio na mkakati wa uenezaji kuhusu usaidizi wa Halmashauri kwa jamii.

***Tokeo Na. 4***


- Kutambua vigezo muhimu vya kuandaa modeli ya O&OD katika Halmashauri lengwa.
- Kuandaa mitazamo mbalimbali ya uenezaji wa Mradi wa O&OD na kufanya uchambuzi wa vigazo muhimu kulingana na mitazamo hiyo.
- Kuanzisha na kuchukua hatua stahiki ili kutimiza vigezo vya uenezaji wa modeli ya O&OD.
- Kubadilishana uzoefu kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotekeleza Mradi na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vijiji nje ya Mradi.



## *Modeli ya O&OD*




### *Muundo wa Mradi*




Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Ofisi ya Mradi wa O&OD
OWM-TAMISEMI (Jengo Jipya) , Dodoma
(P. O. Box 509, Dodoma)

Tel: 026 232 3660
Fax: 026 232 3661
E-mail: pmoralg.ood@gmail.com

*Imetayarishwa na timu ya O&OD*

*2013.05.05*



# KUIMARISHA UPANGAJI MIPANGO SHIRIKISHI JAMII KWA AJILI YA MCHAKATO WA MAENDELEO YAO ILI KUHAKIKISHA UPATIKANAJI WA UTAWALA BORA

# (MRADI WA O&OD)

## *Usuli Wa Mradi*

Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma umekuwa ni changamoto kwa Serikali ya Tanzania kwa miongo mingi sasa. Serikali imechukua hatua kubwa na hasa kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1990 ili kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapewa uwezo kupitia ugatuaji wa majukumu ya kifedha, kuwianisha masuala ya kisheria, na kujitegemea kwenye masuala ya rasilimali watu. Program ya Uboreshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRP:2000-2008) ilikuwa ni moja kati ya juhudi zilizochukuliwa ili kuongeza kasi ya ugatuaji wa madaraka kwa umma. Awamu ya pili ya Programu ambayo inatekelezwa inayoitwa Programu ya Uboreshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa II (LGRP II), ni nguzo muhimu ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na uwezo wa uongozi na uratibu wa maendeleo ya kiuchumi ya jamii ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa huduma zinazotolewa kwa watu kwa ajili ya kuwaletea maisha bora.

Sambamba na Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa, Mchakato wa upangaji mipango kwa kutumia mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD)ulianzishwa mwaka wa 2002 ili kuziwezesha jamii kupanga, kutekeleza na kumiliki mipango yao kwa lengo la kubadili mchakato wa upangaji mipango uliozoeleka nchini wa kutoka juu kwenda chini na kuwa wa kutoka chini kwenda juu. Toka mfumo ulipoanzishwa, hadi sasa serikali imewezesha uenezaji wa mchakato wa O&OD kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa zaidi ya asilimia 90. Kwa sasa Mfumo wa O&OD umeingizwa ndani ya Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa II na unakuwa ni sehemu muhimu ya mchakato wa kukuza/kuimarisha ushiriki wa watu katika shughuli za maendeleo, uwajibikaji na uwazi katika mambo ya utawala bora.

Kutokana na mantiki hii, OWM-TAMISEMI imeamua kuanzisha mradi mpya ujulikanao kama "Kuimarisha upangaji mipango shirikishi jamii kwa ajili ya mchakato wa maendeleo yao ili kuhakikisha upatikanaji wa utawala bora" ili kuuboresha zaidi mfumo wa O&OD. JICA inaisaidia OWM-TAMISEMI katika kuutekeleza mradi huu mpya kama inavyoonyeshwa kwenye makubaliano yaliyowekwa saini na pande hizi mbili mwezi wa Julai, 2009.


## *Malengo ya Jumla*

Mchakato wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo unaboreshwa ili uwe thabiti kwa lengo la kupata mafanikio ya kweli ya kupewa madaraka/Utawala Bora kupitia Maendeleo Shirikishi Jamii Asilia

## *Madhumuni ya Mradi*

Kuandaa Modeli madhubuti zitakazofanikisha mchakato wa O&OD katika ngazi ya Jamii, Kata na Wilaya

## Mahusiano Madhubuti miongoni mwa Matokeo




### Muda wa Mradi

Kuanzia mwezi wa Oktoba, 2009 hadi mwezi wa Oktoba, 2014

### Mamlaka ya Utekelezaji

- Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI)
- Mikoa ya Morogoro na Pwani
- Mamlaka za Serikali za Mitaa 5 zilizochaguliw (Bagamoyo, Kisarawe, Kilombero, Morogoro Vijijini na Ulanga
- Vijiji 10 vilivyochaguliwa kutoka katika halmashauri

### Mamlaka za Uratibu

- Kukundikazi cha mafunzo kwa ajili ya Tokeo 1
- Vikundikazi cha Wilaya kwa ajili ya Matokeo 2,3,4

### Eneo Lengwa

